https://dspace.org/

# Kugeuza Dira ya Toponimi ya Swahili: University of Kabianga holds its first Virtual Graduation Ceremony.

**Karama, Mohamed**

**2021-06**
University of Kabianga
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/418

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

The University of Kabianga
Newsletter
ISSUE NO.5
ISO 9001:2015
Certified Institution
Quarterly Publication from the Office of the Vice-Chancellor
JUNE, 2021

# University of Kabianga holds its first Virtual Graduation Ceremony.

## ation Ceremony Pictorial, 24th March,2021



Procession Ceremony led by student leaders headed to graduation square/ **Photo Emmanual Rotich**



Some of the UoK Council Members during the 8th Graduation Ceremony / **Photo Emmanual Rotich**



Prof. Wilson Kipngeno-VC, introduces members of staff to PS. Amb. Simon Nabukwesi/ **Photo Emmanual Rotich**



From left Amb. Simon Nabukwesi PS University Education ,Center Mr. Mayaka Member of Council and to the right Prof Wilson Kipngeno UoK VC, -During UoK 8th Graduation Ceremony. / **Photo Emmanual Rotich**



Amb. Simon Nabukwesi PS University Education, during his address at UoK 8th Graduation Ceremony /**Photo Emmanual Rotich**



University Education PS. Amb. Simon Nabukwesi, plants a tree during UoK 8th Graduation ceremony. **Photo Emmanual Rotich**

## Highlights

Joining University during the Pandemic

Editorial

Season with reasons

Kugeuza dira ya toponimi ya Swahili

INNOVATION AND EXCELLENCE

### Kugeuza ḏira ya toponimi ya 'Swahili'

Kati ya sahil (ya Ki-Arabu), swahili (ya KiSwahili Sanifu), suaheli (Krapf, 1840), sawahili (Khalid, 1977; Hijazy & Mzenga, 1977), siwahili (Attas, 2018), na ziwahili (ufafanuzi wa mitaani Mambasa) tushike ipi nriyo toponimi (majina ya mahali kionomastiki) ya mwafaka kuhusu mahali watʰu wanaoishi katika upwa wa Mashariki ya Afrika kuṯoka Somalia haḏi Msumbiji? Makala haya mafupi yaṯajaribu kugeuza ḏira ya maelezo kuhusu nyusuli za toponimi ya 'swahili' kuṯoka kulekezwa baharini haḏi kulekezwa barani nrani.

Mengi ya yanayoelezwa kuhusu usuli wa WaSwahili, miji na lugha yao, ni kwamba wameṯokana na kwingiliyana kwao na Waarabu bali kuna wanaosema hii lugha ni uṯanzu mmoja wa lugha ya Ki-Arabu. Kazi nyingi za kianthropolojiya kuhusu WaSwahili zawaonesha kuwa watʰu wanaojishughulisha zaiḏi na bahari ya Hinḏi, kwa uvuvi au biyashara (kwa mfano, Middleton (1992)). Hoja hii nriyo inayosababisha waṯaalamu wengi au pengine woṯʰe kusema kuwa 'swahili' ni neno la Ki-Arabu lenye maana ya 'pwaa ya bahari' na piya laweza kumaanisha watʰu wanaoishi katika ufuwo huu wa Afrika Mashariki (Chiraghdin na Mnyampala, 1977).

Maoni ya Pawlowicz (2012) kwamba tʰwangaliye nrani ya Afrika badala ya kulekeya baharini kuwanasibisha WaSwahili yanaṯokana na uṯafiṯi wake Mikindani, Kusini mwa Tanzania ambao unashahadiya kuwa ṯʰimbo nyingi za huko zaonesha ni mji uliyoṯangamana zaiḏi na bara kuliko pwani. Maoni haya yanatiliya nguvu kazi ya Nurse na Spear (1985) inayoshaḏiḏiya kuwa ushahiḏi wa vifaa na magaye yaliyoṯafiṯiwa katika miji ya pwani ya Afrika yakilinganishwa na data ya kilugha yanaonesha kuwa WaSwahili asili zao ni watʰu wa Afrika nrani waliyohama haḏi kufikiya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki.

Kulingana na kazi za Nurse na Spear (khj.) na *Mapisi ya WaSwahili* ya Marehemu Ahmad Nabhany (2011) zinaonesha kuwa WaSwahili ni watʰu wanaozungumza Ki-Bantu wanaoṯokeya katika kunri kubwa la wasemaji wajulikanao Niger-Congo ambalo asili yake ni Afrika Magharibi. Wazo hili la Niger-Congo na lile la Pawlowicz (khj.) la kwangaliya usuli wa WaSwahili nrani bara linatufanya tuchukuwe msimamo mpya kuhusu toponimi ya 'swahili' kwamba inaṯokana na bara kuliko inavoaminika hivi sasa katika mawanḏa ya mapisi na anthropolojiya ya WaSwahili.

Mosi, katika makala ya Suleiman (2017) kwenye jariḏa la *The Conversation* anaeleza kwamba 'sahel' (piya huṯamkwa 'sahil') ni eneo liko kusini mwa Jangwa la Sahara linalojumuisha nchi kwanziya Senegal, Mauritania, Mali, Burkina Faso, Niger, Nigeria, Chad, Sudan, mpaka Eritrea. Anaongeza kuwa eneo hili la 'sahel' kiuṯamaduni na kihistoriya ni mwambao baina ya Mashariki ya Kati na nchi za kusini mwa Sahara. Pili, Jacques (1837), akinukuliwa katika wikipedia, anasema kuwa 'sahil' kwa maana ya 'ufuwo' ni kiuṯamathali wa lugha na katika Kamusi ya Al Mawrid (1995) kwa Ki-Arabu cha Kikale ina maana ya 'ardhi ṯambarare'

maelezo yanayoafiki ufafanuzi wa Schoff (1912) akinukuliwa na Hinnebusch (1996:92) kwamba hii miji ya Uswahilini ni 'nyangwa k$^{h}$avu za pwani kusini mwa Mṯikati'. Tuṯaona kuwa neno 'jangwa' haliyepukiki katika ufafanuzi wa neno 'swahili'. Haṯa 'nyangwa' kwa Ki-Swahili ina maana ya 'ardhi ṯambarare ilopakana na bahari'. Kwa hivo, kauli za Nurse na Spear na Nabhany kuhusu Niger-Congo ni sahihi kuwa WaBantu asili yao ni Afrika Magharibi na neno walilotumiya kujitambulisha nako ni 'swahili'.

Pengine mṯafiṯi aweza kuuliza neno lililosemwa ni 'sahel/sahil' na wala si 'swahili'. Haya yanapatikana katika lugha ya Ki-Swahili kwa kudonrosha au kwengeza sauṯi katika maneno, kwa mfano, katika neno hili pameengezwa /w/. Katika lahaja za Ki-Swahili /s/ na /sw/ huweza kupatikana katika neno na isibadilishe maana ya neno hilo. Kwa mfano, maneno /swi/ Ki-Vanga huṯamkwa /isi/ katika lahaja za Kaskazini – Mambasa mpaka Kiunga – kwa maana ya 'samaki'. Piya wako Wamviṯa wanaosema /swiswi/ kurejeleya /sisi/ (*us*, Kiingereza) katika KiSwahii Sanifu. Haṯa maṯamshi ya sāḥil ['sa:ħil] 'ufuwo wa bahari' na sahl 'ardhi ṯambarare' inaṯafauṯiyana; ya pili yafanana zaidi na 'swahili' ya KiSwahili Sanifu. Hivo basi, kwa kuita miji yao 'swahili' (au, kisisi, 'sahili') ni kushahaḏiya kwamba waṯoka bara katika nchi k$^{h}$avu za jangwani.

Kwa ufupi, makala yet$^{h}$u yameonesha maṯamko ṯafauṯi ṯafauṯi ya neno 'swahili' kurejeleya miji iliyopakana na upwa wa Afrika Mashariki. Tumerejeleya mawazo ya waṯaalamu wa Anthropolojiya na Chimbo kuhusu unasibishaji wao wa neno hili na uṯamaduni wa WaSwahili kulekeya baharini, haswa ya Hindi. Walakini, kuṯokana na ushahiḏi wa Kimachimbo na magaye ya miji ya WaSwahili na ushahiḏi wa lugha ya Ki-Swahili na Ki-Bantu, kwa upana, tumeṯowa wazo jipya kuhusu neno hilo 'swahili'. Usuli wa toponimi yake yaonesha neno hilo lafaa liyelekezwe Afrika barani kuliko kulekezwa baharini kwa sababu usuli wa neno hilo ni 'sahili' inayomaanisha ardhi k$^{h}$avu kusini mwa Sahara. T$^{h}$waamini kwa kutumiya ṯaaluma hii ya toponimi kwangaziya nyusuli za majina ya miji iliyomo katika eneo hili t$^{h}$waweza kupata ushahiḏi zaiḏi kuhusu geuko la ḏira yetu kuṯoka baharini haḏi barani.

Dkt. Mohamed Karama,
**Idara ya Isimu Lugha na Mawasiliyano**

